THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021 **KISWAHILI**
(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni tu)

Muda: Saa 3 **Jumanne, 05 Novemba 2013 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.

3. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU A (Alama 10)
UFAHAMU
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

Ima mwana wende kasi, ima usirudi nyuma
Ima ukwepe sabasi, ima ukipite kima
Ima ujivike lasi, ima ndiyo taadhima
Ima mwanakwetu ima, dunia ni sarakasi.

Ima kasema **mkwasi**, ima uende kulima
Ima njaa sikughasi, ima mgongo inama
Ima wepuke uasi, ima upate usalama
Ima mwanakwetu ima, ima ndipo utapasi.

Ima ndipo **utapasi**, ima mwanakwetu ima
Ima ujiunge nasi, ima tuujenge umma
Ima usile najisi, ima ule cha kuchuma
Ima mwanakwetu ima, ima emaye hakosi.

Ima emaya hakosi, ima **jikalifu** ima
Ima upweke tatasi, ima wewe na Mwajuma
Ima yoyomea kusi, ima usiuye nyuma
Ima wa ima faima, ima upate fulusi.

Ima wmanakwetu basi, ima usende kinyuma
Ima kazi ni **libasi**, ima inama kulima
Ima wacha udadisi, ima nakwambia ima
Ima usikae ima, kama kuishi wahisi.

Maswali

(a) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilolisoma:
   (i) Mkwasi
   (ii) Utapasi
   (iii) Jikalifu
   (iv) Libasi

(b) Kwa kutumia sentensi tatu (3), fafanua ujumbe wa mwandishi katika shairi hili.

(c) Msanii ana maana gani anaposema “Ima mwanakwetu ima, dunia ni sarakasi.”

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha fupisha habari hii kwa maneno hamsini (50).

Kijana anahitaji kuwa na rafiki ili aweze kuondokana na ukiwa pia ili aweze kupata faraja. Aidha hayo yatajitokeza kwa sababu atafahamiana na marafiki hao, vilevile atazoeana nao hasa kwa kupitia maongezi. Kijana huweza kupata marafiki popote, kwa mfano miongoni mwa majirani zake, shuleni,

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

kazini, sehemu za ibada na hata awapo safarini. Lakini kijana anapaswa kuwa mwangalifu katika kuchagua marafiki.

Katika makuzi yake kijana huwa karibu sana na rafiki zake ambao kwa kiasi kikubwa huwa na nguvu na ni rahisi kwa rafiki kuambukizana tabia ambazo zaweza kuwa nzuri au mbaya. Kwa hiyo ni jukumu la wazazi kumwelekeza kijana na kumshauri kuhusu ni yupi hasa rafiki mwema. Ni heri kukosa rafiki kuliko kuwa na rafiki mlevi, mwongo, mwizi, mvivu, mvuta bangi au mtumiaji wa dawa za kulevya. Rafiki mzuri ni yule mwenye tabia njema na busara ambaye hutoa ushauri mzuri unaoweza kumsaidia mtu kupata mafanikio katika maisha.

SEHEMU B (Alama 25)
SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kuzingatia tungo ulizopewa, bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari:
   (a) Juzi tulishiriki maandamano ya amani.
   (b) Kucheza kwake kunaburudisha.
   (c) Kijana mlevi amepata ajali.
   (d) Hamisi alikuwa amekwisha kwenda kulima.
   (e) Wale vikongwe wamepata msaada.
   (f) Mawazo hayo si yangu.
   (g) Sitakwenda kwake asilani!
   (h) Amekwenda kazini ijapokuwa ni mgonjwa.
   (i) Hiki kitawekwa ukumbini.
   (j) Mbuzi amekwisha kata kamba.

4. Unganisha tungo zifuatazo kwa kutumia O-rejeshi:
   (a) Mafisadi wamekamatwa. Mafisadi wamefikishwa mahakamani.
   (b) Kitabu kimenunuliwa. Kitabu kipo kabatini.
   (c) Mfadhili amepatikana. Mfadhili mkarimu sana.
   (d) Hukumu imetolewa. Hukumu ni ya haki.
   (e) Mahali pameandaliwa. Mahali hapatoshi.

5. Bainisha kauli zinazowakilishwa na vitenzi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo:
   (a) Refa alichezesha mechi vizuri.
   (b) Mtoto amevunjwa mguu.
   (c) Wanafunzi wanasomeana kitabu.
   (d) Mafuta yamemwagika.
   (e) Walevi wanapigana kilabuni.
   (f) Mtoto analia sana.
   (g) Babu alisomewa kitabu.
   (h) Dada anampikia mtoto uji.
   (i) Kaka alimtuliza rafiki yake.
   (j) Gazeti linasomeka vizuri.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

6. Vishazi tegemezi hufanya kazi ya vivumishi viwapo katika tungo. Onesha ukweli wa kauli hiyo kwa kutumia mifano minne ya sentensi.

7. Toa maana ya kamusi kisha fafanua sehemu kuu tatu zinazounda kamusi.

SEHEMU C (Alama 10)
UANDISHI
Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Wewe ni Kiranja Mkuu wa Shule ya Sekondari Kazamoyo iliyoko Tanga, jina lako Uwezo Jitihada na unasoma kidato cha nne. Andika barua kwa Mkuu wa Shule ukiomba ruhusa ya kuhudhuria semina ya uelimishaji rika takayofanyika tarehe 10/11/2013 katika Shule ya Sekondari Tutafika iliyoko Moshi. Barua yako ipitie kwa Mwalimu wa Darasa.

9. Jifanye wewe una elimu ya kidato cha nne, jina lako Situmai Kasheshe unayeishi kijiji cha Songambele kilichopo wilayani Mpanda. Tumia taarifa zilizomo kwenye tangazo lifuatalo lililotolewa kwenye gazeti la Mwananchi la tarehe 01/12/2013 kuandika barua ya maombi ya kazi.

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Kazi: Karani Masijala
Sifa:

- Awe amehitimu kidato cha nne na kufaulu masomo ya Kiingereza na Hisabati
- Awe na umri usiozidi miaka 35
- Awe Mtanzania
- Awe na ujuzi wa kompyuta

Barua ya maombi iambatanishwe na nakala za vyeti na itufikie kabla ya tarehe 15/12/2013.

Maombi yote yatumwe kwa:

Afisa Mwajiri
Kampuni ya Kutengeneza Masufuria
S.L.P 600
KATAVI.

SEHEMU D (Alama 10)
MAENDELEO YA KISWAHILI
Jibu swali la **kumi (10)**

10. Kwa kutumia hoja tano zenye mifano, eleza kwa kifupi mchango wa wamisionari wa kikristo katika kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru.

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU E (Alama 45)
FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

11. Kwa kutumia mifano, fafanua dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika fasihi:
    (a) Tashibiha
    (b) Takriri
    (c) Sitiari
    (d) Tashihisi
    (e) Tanakali sauti
    (f) Tasfida

12. "Mtunzi wa mashairi huibua malalamiko ya kundi la wasionacho." Fafanua kauli hiyo kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma.

13. "Mapenzi ya dhati huleta faraja miongoni mwa wanajamii." Tumia hoja tatu kutoka katika kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma kuonesha jinsi wahusika wake walivyofarijika na mapenzi ya dhati

14. Onesha kufaulu kwa dhamira za msanii kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila tamthiliya kati ya tamthiliya mbili ulizosoma.

15. Eleza maana ya ngano kisha tunga ngano yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) na yasiyozidi mia nne (400).

ORODHA YA VITABU

Ushairi		
Wasakatonge	-	M.S. Khatibu (DUP)
Malenga Wapya	-	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	-	T.A Mvungi (EP& D.LTD)
Riwaya		
Takadini	-	Ben Hanson (MBS)
Watoto wa Maman'tilie	-	E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu	-	A.J. Safari (H.P.)
Tamthiliya		
Orodha	-	Steve Reynolds (MA)
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe	-	E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu	-	Medical Aid Foundation (TPH)

Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org